

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**1. **Insha ya lazima.**

1. Andika dayalojia baina yako na kiongozi wa nyumba kumi kuhusu jinsi ya kuimarisha usalama katika eneo lenu.
2. Simu tamba, kiungambali, rununu au simu sogezi zina faida na hasara yake. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali; Hisani haozi.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno; ... niliaibika. Nilipopiga darubini nyuma na kutafakari kuhusu kitendo nilichotenda, nilitamani ardhi ipasuke nitumbukie huko nisionekane tena.

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**1. **UFAHAMU** (alama 15)**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Watahiniwa na wanafunzi wengine wanapoendelea kujiandaa kwa mitihani yao hasa wakisubiri ule wa mwisho, wanatumia mbinu mbalimbali katika kujiandaa huko. Mojawapo ya mbinu bora ya kutumia ni ile ya makundi. Mbinu hii huhusu kuwaweka wanafunzi katika makundi mbalimbali ili wayatumie katika udurusu wao.

Aghalabu, mwalimu huongoza shughuli hii ambapo hutumia uwezo wa wanafunzi katika kupanga makundi hayo. Hili huwa muhimu kwa kuwa huwafanya wanafunzi wanaoonekana kuwa na uwezo wa chini kujumuika na wale wanaoonekana kuwa wenye uwezo wa juu. Hata hivyo, huwa ni muhimu kujaribu kusawazisha makundi hayo ili wanafunzi wa kiwango cha juu wasione kuwa wanapoteza wakati wao na kwamba wanawafaidi wengine bila wao kufaidi. Hivyo basi, hulazimu kuwa na wanafunzi wawili wa viwango mbalimbali ili wote wanufaike. Idadi ya wanafunzi katika makundi hutegemea idadi yao, uwezo na mtazamo wa mwalimu wao. Yafuatayo ni baadhi ya manufaa.

Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, huwa na uhuru zaidi wa kuchangizana na kuelezana wanayoyajua. Hufanya hili bila uoga ambao wanaweza kuwa nao hasa mwalimu anapokuwa darasani. Imebainika mara nyingi kuwa, mwanafunzi anaweza kuelewa au kulijua jambo fulani, lakini akakosa kulisema au kutoa mchango wa jambo hilo darasani anapoulizwa na mwalimu. Sababu huwa tofauti tofauti kama vile uoga, kutokuwa na uhakika, kutotaka kusikika, n.k. Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, haya hayajitokezi na huonekana wakizungumza kwa wazi na ukakamavu. Hivyo basi, husema wayajuayo, na kuwapa wanafunzi wenzao uwezo wa kuyasikia na kuyakosoa mawazo yao. Aidha, ikiwa watataka kunyamaza makundini, wenzao watasisitiza kuwa watoe maoni yao, na kuchangia kuhakikisha kuwa wananoleka ifavyo. Wanafunzi wanapokuwa katika vikundi, huwa na uhuru wa kusema kuwa hawalijui jambo fulani, na kutoa fursa kwa wenzao kuwauani. Wanapojadili suala fulani, kila mmoja hutoa mtazamo wake, wakajumuisha pamoja na kuishia kuyajua mengi zaidi kuliko walivyojua mwanzoni. Huwa si ajabu kuona wanafunzi wanaoonekana kuwa dhaifu wakiwa makini kusikiliza na kusaidiwa, wakaanza kuelewa mambo kwa njia bora zaidi kuliko walivyoelezwa na mwalimu. Kwa kufanya hivyo, huwa na uhuru wa kuwaomba wenzao warudie maelezo fulani na kufafanuliwa polepole, wakaelewa kuliko walivyoelezwa na mwalimu.

Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, wanaweza kupewa suala fulani kujadili. Wanapopewa vitabu wanaweza kutathmini yaliyojadiliwa na kubaini makosa. Wanaweza kujiuliza mbona masuala fulani hujitokeza jinsi yaliavyo katika vitabu hivyo. Mfano mzuri katika shule za upili ni baadhi ya maelezo yanayokanganya katika baadhi ya vitabu kuhusu masuala kama vile vitenzi na virai, ambapo wanafunzi wanaweza kuyaangazia katika makundi na kubaini utata unaojitokeza. Hii ni mbinu bora ya kujihakikishia uelewa bora. Vilevile, wanafunzi wanaweza kubaini mengi wakichambua vitabu vya fasihi kwa pamoja, ambapo wanaweza kubaini masuala mengi ambayo huenda mwalimu hakuyadadavua. Wengi hujitokeza kubaini makubwa na madogo katika vitabu hivi. Pia, wanaweza kuwa na vitabu mbalimbali vinavyoeleza masuala yanayojadiliwa, na kusaidia kupata mambo mengi zaidi.

Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, huhimizana kuzungumza na hivyo basi wale ambao kwa kawaida huwa waoga wakaanza kupata ujasiri. Wanaweza kuanza kuchangia mara moja moja, na kadri wanavyozoeana makundini ndivyo wanavyozidi kuzungumza zaidi, wakajitokeza kuwa jasiri zaidi. Hili hasa huzidi huonekana kwa kuwa, wao kupata himizo kutoka kwa wenzao. Ili kuhakikisha kuwa ujasiri huo umekuzwa kabisa, mwalimu anafaa awaelekeze wanafunzi mbalimbali wa vikundi hivyo kuwasilisha hoja zao mbele ya wenzao. Ni muhimu wanafunzi waelewe kuwa kila mmoja wao atapata fursa ya kuwasilisha mbele ya wenzao, ili waimarike kabisa.

Wanafunzi, wanavyozidi kuwa pamoja ndivyo wanavyozidi kuzoeana na kuishia kuwa marafiki wa toka nitoke. Wao huendelea kukurubiana katika masuala mbalimbali. Aidha, mwalimu anaweza kuzua mashindano baina ya makundi, yatakayowalazimu wanafunzi kuhusika kwa karibu zaidi na kushirikiana kuhakikisha wanaibuka kuwa bora.

**Maswali.**

1. Toa anwani mwafaka ya kifungu ulichosoma. (alama 2)
2. Kuna umuhimu gani kwa mwalimu kuutumia uwezo wa wanafunzi anapopanga makundi? (alama 2)
3. Idadi ya wanafunzi katika kila kikundi hutegemea mambo yapi? (alama 3)
4. Eleza manufaa ya kujifunza kwa mbinu inayozungumziwa katika makala haya. (alama 4)
5. Ujasiri wa mwanafunzi unaweza kukuzwa vipi? (alama 2)
6. Eleza maana ya maneno haya jinsi yalivyotumiwa; (alama 2)
  - (i) Marafiki wa toka nitoke.
  - (ii) udururu

2. **UFUPISHO (alama 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Watu wengi, wanaamini kwamba kufundisha watoto nyimbo shuleni ni kupoteza wakati unaofaa kwa masomo ya maana. Lakini muziki nyumbani na shuleni una manufaa mengi.

Muziki ni kitulizo kikubwa sana cha moyo wa binadamu. Muziki una njia ya kipekee ya kuwasiliana. Baadhi ya ujumbe hauwezi kupitishwa kwa njia nyingine ila kwa muziki.

Muziki umetajwa kumsaidia mtoto kwa mambo yafuatayo:

Kuendelea hisia nzuri, za kuburudisha na kuzuzua. Muziki humsaidia mtoto kuweza kukabiliana na tajriba mbaya. Unampa fursa ya kutoa moyoni simanzi na dhiki yake na hivyo kumrejeshea raha tana. Liwazo la muziki ni dhahiri wakati mtoto anapolala pindi anapoiambiwa bembelezi.

Inaaminika pia kwamba muziki unakomaza akili ya mtoto na ni nyenzo muhimu sana katika hafla yake ya kujifanyia mambo, hasa kwenye miaka yake ya mapema. Muziki huhitaji umakinifu ili kutambua miondoko na maneno halisi ya wimbo huo na mambo haya humfanya mtoto kuhamisha umakini huu kwenye masomo mengi darasani. Inaaminika pia kwamba kupitia kwa muziki mtoto anaweza kujifunza mbinu ya kukumbuka mambo anayofunzwa masomoni.

Watoto ambao hujifunza muziki mara kwa mara hujipatia mbinu za werevu shuleni haswa kwenye somo la hesabu na werevu wa mambo mengine kwa jumla. Utafiti umeonyesha kwamba watu wazima ambao walijifunza muziki kabla wafikishe umri wa miaka kumi na mbili huwa na utumizi mzuri wa maneno magumu na msamiati kuliko wale ambao hawakujifunza kuimba.

Muziki pia husaidia watoto walio na kasoro za kuzungumza au walio na ulimi mzito wa kuzungumza. Watoto au watu wazima walio na shida ya kigugumizi huweza kujieleza kwa ufasaha kwa kupitia muziki na jambo hili huboresha kujiamini kwao kwa kibinafsi. Watoto kama hao huweza kujifunza na kuelewa mila na tamaduni zao.

**Maswali.**

- (a) Dokeza mambo muhimu yaliyomo katika aya ya kwanza hadi ya tatu. (maneno 50 - 55)
- (b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa kuzingatia manufaa ya kujifunza muziki. (maneno 65 - 70) (alama 6, utiririko 1)

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)

1. Tofautisha sauti /th/ na /dh/ (alama 2)
2. Ainisha viambishi tamati katika tungo lifuatalo; (alama 2)
 

Waliombewa
3. Tunga sentensi ya neno moja yenye visehemu vifuatavyo; (alama 4)
  - (i) Kiambishi kikanushi
  - (ii) Kiambishi cha hali timilifu.
  - (iii) Kiambishi cha mtendewa.
  - (iv) Mzizi wa kitenzi
  - (v) Kauli ya kutendea
  - (vi) Kitamatishi
4. Onyesha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
 

Mhudumu mmoja awalettee gilasi ya maji.
5. Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo; (alama 2)
 

Kasisi alipoingia kanisani, waumini walianza kushangilia.
6. Bainisha matumizi ya 'ni' katika sentensi; (alama 2)
 

Rudini uwanjani mkanitafutie vikombe ambavyo ni vya kunywea chai.
7. Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi hii; (alama 2)
 

Kitabu chochote kitafaa kwa kazi ii hii.
8. Tumia kiambishi 'ji' katika fungutenzi ili kuleta dhana na kurejelea kiima. (alama 2)
 

Vilevile kitumie kama kiwakilishi cha nafsi ya pili.
9. Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali; (alama 4)
 

Alienda usiku ingawa nilimtahadharisha.
10. Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa; (alama 3)
 

"Mtaweza kumsaidia mtoto wangu kesho?" mzazi akamuuliza mhisani.

11. Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)  
 (i) - la (kauli tendeshea)  
 (ii) Toa (tendeka)
12. Eleza matumizi ya alama zifuatazo za uakifishi. (alama 2)  
 (i) Alama ya hisi  
 (ii) Parandesi
13. Andika katika ukubwa wingi; (alama 2)  
 Ngoma hii itachezwa uwanjani
14. Andika katika wingi karibu; (alama 2)  
 Kijakazi yuyo huyo aliupoteza ufunguo uo huo licha ya kukanywa.
15. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali ya -a- (alama 2)  
 Chui hula swara.
16. Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari. (alama 2)  
 Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na viongozi wenye misimamo thabiti mno.
17. Tumia 'O' rejeshi tamati; (alama 1)  
 Kiatu kinachonunuliwa si kile unachotaka.
18. Yakinisha sentensi hii katika nafsi ya tatu umoja (alama 2)  
 Tusipoonana na wazazi hatutapata pesa

4. **ISIMUJAMII.(alama 10)**

**Soma kifungu kinachofuata kisha ujibu maswali vanayofuata.**

Aliyenaswa na pembe 50 za ndovu ashtakiwa.

Mwanamume aliyekamatwa akiwa na pembe 50 za ndovu katika nyumba yake mtaani Githurai alishtakiwa kwa makosa mawili ya kupatikana na bidhaa za wanyama pori.

**Maswali**

- (i) Bainisha sajili ya makala haya. (alama 2)  
 (ii) Eleza sifa za sajili uliyoitaja kwa ujumla. (alama 8)

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016**

102/3

**KARATASI YA TATU****FASIHI****SEHEMA YA A: USHAIRI**1. **Lazima.****Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.(alama 20)**

Natwaa hino nafasi, lilo tanza kukariri,  
Nayafichua upesi, ambayo kamwe si siri,  
Msikize nyinyi mbasi niwapashe i habari,  
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Kuntu ndaningu nafsi, likanipa tafakari  
Mechunguza si kiasi, katanabahi dosari,  
Ndipo miye nikahisi, kuliamba kwa hiari,  
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Kila siku Jumamosi, Dominika desturi,  
Magazeti binafusi, nashufu kila nahari,  
Watunzi wote sisizi, ndisi wavuli mahiri,  
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Nikatwaa karatasi, na peni yangu saghiri,  
Niongozwe na Kudusi, kasarifu mistari,  
Na pasipo wasiwasi, nudhumu hino sawiri,  
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Swala ninaloakisi, muda mwingi limejiri,  
Nalunga sifanyi kesi, ingawa ni taksiri,  
Haya yaso ufanisi, wadhiha yamekithiri,  
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Mlo kike mwatughasi, kutoshiriki dhahiri,  
Talanta mnazo basi, ila hamwonyeshi ari,  
Umalenga u kuasi, ni wazi ja meno ngiri,  
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Beti nane za utesi, zanisemesha kwa heri,  
Kuwashutumu sikosi, yamo murwa yakijiri,  
Nitiye habta kasi, miye shaha machachari,  
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

**Maswali.**

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 2)
- (b) Taja bahari mbili zinazojitokeza katika shairi hili kwa kuzingatia; (alama 2)
- (i) Vina
- (ii) Mishororo
- (c) Thibitisha kuwa shairi hili ni la kiarudhi. (alama 4)
- (d) Eleza maudhui yanayojitokeza katika ubeti sita. (alama 2)
- (e) Bainisha toni ya mshairi. (alama 2)
- (f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (g) Toa mifano miwili inayoonyesha idhini ya mshairi. (alama 2)
- (h) Eleza maana ya maneno haya;
- (i) mwatughasi
- (ii) utesi

**SEHEMU B: RIWAYA.****Ken Walibora: Kidagaa Kimwemwozea.****Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Basi leo ni leo asemaye kesho ni mwongo ..."  
"Atakiona cha mtema kuni."
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

(alama 4)

- (b) Eleza mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
- (c) Kwa kutoa mfano eleza jinsi suala la uozo wa viongozi linavyojitokeza katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 14)
3. Kwa kutolea mifano mwafaka eleza jinis mbinu zifuatazo zimetumika kufanikisha riwaya ya Kidagaa kimemwozea. (alama 20)
- (i) Sadfa
- (ii) Jazanda

**SEHEMU C: TAMTHILIA****Timothy Arege: Mstahiki Meva****Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Tumechoka kuumbuliwa. Miaka yote tuliyoifanya kazi sisi hatuoni matunda yake. Karibu tunastaafu lakini hakuna hazina maana hakuna cha kuweka. Ni kazi ya kijungu jiko!"
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Bainisha tamathali ya usemi uliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
- (c) Tamthilia ya Mstahiki Meva imeangazia harakati za kuleta ukombozi. Fafanua mbinu zilizotumiwa na wanacheneo kujikomboa. (alama 14)
5. "Kama huku si kuwatusi wananchi basi ndio kutembea nyuma ya punda aliyeudhika."
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Eleza mbinu zozote nane ambazo Meva Sosi alitumia ili kuendeleza utawala wake. (alama 16)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI****Ken Walibora na S.A Mohamed (wah): Damu Nyeusi.**

6. "Mwanzoni sikuridhia kwa kuwa nilikuwa kama mtu aliyeona unyasi baada ya kuumwa na nyoka."
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Taja tamathali ya usemi inayobainika wazi katika dondoo hili. (alama 2)
- (c) Eleza nafasi ya mwanamke katika hadithi hii. (alama 10)
- (d) Mbinu ya kinaya imetumika katika hadithi hii. Thibitisha. (alama 4)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.**

7. (a) Eleza maana ya maigizo. (alama 2)
- (b) Tofautisha aina mbili kuu za maigizo. (alama 4)
- (c) Kwa kutoa hoja **nne** eleza umuhimu wa maigizo. (alama 4)
- (d) Eleza dhima ya nyiso. (alama 10)